# هذه دعوتنا وعقيدتنا

## *Hii ndio Da´wah na ´Aqiydah yetu*

*Mwandishi:* **´Allaamah Muqbil bin Haadiy al-Waadi´iy**

*Tarjama* [*na maelezo*]: **Abu Bakr Khatwiyb al-Atrush**

بسم الله الرحمن الرحيم

1- Tunamuamini Allaah kwa majina na sifa Zake kama ilivyotajwa katika Kitabu cha Allaah na Sunnah za Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam)[1], pasi na upotoshaji[2], kufasiri kimakosa, ufananishaji, ushabihishaji[3] wala ukanushaji.

2- Tunaamini kuwa kuwaomba maiti na kuwataka msaada - hata walio hai katika mambo wasiyoyaweza isipokuwa Allaah - ni kumshirikisha Allaah.

3- Kuwa na imani juu ya hirizi ya kwamba inanufaisha pamoja na Allaah au yenyewe ni shirki. Kuivaa bila ya kuwa na imani yoyote juu yake ni ukhurafi.

[1] Imaam Swaalih bin Fawzaan al-Fawzaan (Hafidhwahu Allaah) amesema:

"Majina na Sifa za Allaah ni kukomeka (Tawqiyfiyyah), ikiwa na maana ya kwamba yanathibitishwa tu yale yaliyotajwa katika Qur-aan na Sunnah. Kwa hivyo hatumvumbulii Allaah Majina wala Sifa mpya. Hatumsifu kwa jengine isipokuwa yale yaliyotajwa katika Qur-aan na Sunnah na wala hatumpangii jina ambalo halikuja katika Qur-aan wala Sunnah. Hii ndio maana ya kukomeka." (Sharh ad-Durrah al-Madhiyyah, uk. 76-77).

[2] Takyiyf. Imaam ´Abdul-´Aziyz bin ´Abdillaah bin Baaz (Rahimahu Allaah) amesema:

Wakati Imaam Maalik (Rahimahu Allaah) na wengineo katika Salaf walipoulizwa juu ya hili - yaani namna Allaah alivyolingana - wakasema:

"Kulingana kunajulikana, namna haijulikani, kuamini hilo ni wajibu na kuuliza juu ya hilo ni Bid´ah."

Bali Yeye (Subhaanahu wa Ta´ala) ni mwenye kusifika kwa sifa, kama alivyoeleza Mwenyewe, bila ya kuzidisha wala kupunguza. Nazo ni sifa za kihakika. Kulingana ambako ni kwa hakika. Kusikia kwa hakika. Kuridhia kwa hakika. Kukasirika kwa hakika. Sifa zote hazina *Majaaz*. Bali ni za hakika kwa njia inayolingana na Allaah. (Sharh al-´Aqiydah al-Waasitwiyyah, uk. 18-19)

[3] Tashbiyh na Tamthiyl. Imaam Swaalih bin Fawzaan al-Fawzaan (Hafidhwahu Allaah) amesema:

"Kushabihisha na kufananisha ina maana moja na maana yake ni kufananisha Sifa za Allaah na sifa za viumbe. Kwa mfano kusema Mkono wa Allaah ni kama mikono yetu na usikizi Wake ni kama usikizi wetu - Ametakasika Allaah na hilo!" (Sharh al-´Aqiydah al-Waasitwiyyah, uk. 15)

4- Tunachukua udhahiri wa Qur-aan na Sunnah na hatupindishi maana[4] isipokuwa kwa dalili kutoka katika Qur-aan na Sunnah inayopelekea kufanya hivo.

5- Tunaamini kuwa waumini watamuona Mola wao Aakhirah bila ya kuulizia namna[5]. Vilevile tunaamini kuwepo kwa uombezi na kwamba waislamu waliokuwa wakimuabudu Allaah Pekee watatoka Motoni.

6- Tunawapenda Maswahabah wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na tunamchukia yule mwenye kuwasema vibaya[6]. Tunaamini

[4] Ta´wiyl. Imaam Ibn-ul-Qayyim (Rahimahu Allaah) amesema:

"Kwa mujibu wa wafasiri wa Qur-aan na wanazuoni wa Fiqh na Hadiyth katika Salaf, Ta´wiyl maana yake ni "tafsiri" (Tafsiyr) na ubainifu (Bayaan). Kutokana na taarifu hii Ibn Jariyr huwa akisema: "Tafsiri (Ta´wiyl) ya Kauli Yake (Ta´ala) ni kadhaa na kadhaa...

Ama kuhusu uelewa wa Ta´wiyl kwa Mu´tazilah, Jahmiyyah na wanafalsafa wengine, maana yake ni kuyapindisha maneno kutoka katika maana yake iliyoteremshwa kwayo." (Mukhtaswar as-Sawaa´iq al-Mursal, uk. 21).

[5] ´Allaamah ´Abdul-´Aziyz bin ´Abdillaah ar-Raajhiy (Hafidhwahu Allaah) amesema:

"Masuala ya kuonekana kwa Allaah Peponi ni miongoni mwa mambo makubwa ambayo kuna mizozo kati ya Ahl-us-Sunnah na wenye kwenda kinyume nao katika Ahl-ul-Bid´ah. Haya ni kama masuala ya kuzungumza kwa Allaah. Hali kadhalika masuala ya Allaah kuwepo juu ya mbingu na juu ya ´Arshi.

Mambo haya matatu ndio alama tatu zenye kupambanua baina ya Ahl-us-Sunnah na Ahl-ul-Bid´ah. Chukua ndio iwe kanuni yako ya kwamba: yule mwenye kuthibitisha kuwa Allaah ataonekana Aakhirah, akathibitisha Maneno ya Allaah na kwamba anazungumza kwa herufi na sauti na kwamba Maneno ya Allaah yako kwa matamshi na maana na kwamba Allaah yuko juu ya mbingu amelingana juu ya ´Arshi ametengana na viumbe Vyake, basi huyo ni katika Ahl-us-Sunnah. Na yule mwenye kupinga mambo haya matatu basi jua kuwa ni katika Ahl-ul-Bid´ah." (al-Hidaayah ar-Rabbaaniyyah fiy Sharh al-´Aqiydah at-Twahaawiyyah (01/217)

[6] Imaam ´Abdul-´Aziyz bin ´Abdillaah bin Baaz (Rahimahu Allaah) amesema:

"Kadhalika inatakiwa kuamini ya kwamba mbora katika makhaliyfah waongofu ni aswSwiddiyq,kisha ´Umar, kisha ´Uthmaan halafu ´Aliy. Licha ya kwamba kuna baadhi ya watu waliovutana kidogo kama inatakiwa kumtanguliza ´Uthmaan juu ya ´Aliy au kinyume chake. Lakini hatimaye Ahl-us-Sunnah walifikia kuona kuwa kuwa ´Uthmaan ndiye watatu na kwamba ´Aliy ndiye wanne. Hili linahusiana na uongozi na ubora.

Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah wanatakiwa kuamini hivi na wajitenge mbali na mwenendo wa Raafidhwah ambao kazi yao wao ni kuwatukana Maswahabah na kuwafanyia maudhi. Vilevile wanatakiwa kujitenga mbali na mwenendo wa Nawaaswib ambao wanawaudhi watu wa nyumba ya

kuwa kuwatukana ni kuitukana dini. Kwa sababu Maswahabah ndio waliotunukulia nayo. Vilevile tunawapenda watu wa nyumba ya kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) mapenzi ya Kishari´ah[7].

7- Tunawapenda Ahl-ul-Hadiyth na Salaf[8] (wahenga) wa Ummah huu ambao ni katika Ahl-us-Sunnah.

8- Tunachukia elimu ya falsafa[9] na tunaona kuwa ni sababu kubwa ya kufarikisha Ummah.

---

kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kwa maneno na vitendo. Ahl-us-Sunnah wanatakiwa kujiepusha na tabia hii chafu. " (Sharh al-´Aqiydah al-Waasitwiyyah, uk. 116)

[7] Imaam ´Abdul-´Aziyz bin ´Abdillaah bin Baaz (Rahimahu Allaah) amesema:

"Aidha Ahl-us-Sunnah wanaonelea kuwa ´Aliy (Radhiya Allaahu ´anh) ni kamaMaswahabah wengine wote, kwamba yeye ni khaliyfah wa nne ana fadhila zake na kwamba yeye ni mmoja miongoni mwa wale Maswahabah kumi waliobashiriwa Pepo. Pamoja na yote haya hawapitilizi kwake, hawamuombi pamoja na Allaah, hawasemi kuwa amekingwa na kukosea na wala hawasemi kuwa yeye ndiye alikuwa ni mwenye kustahiki utume na kwamba Jibriyl (´alayhis-Salaam) alifanya usaliti. Yote haya ni batili. Lakini wanaona kuwa ni miongoni mwa Maswahabah wabora na wema (Radhiya Allaahu ´anhum). Pamoja na yote haya hawavuki mipaka kwao, hawavuki mipaka kwa Faatwimah (Radhiya Allaahu ´anhaa), al-Hasan na al-Husayn (Radhiya Allaahu ´anhumaa) na wengineo. Bali wanaonelea kuwa yule mwenye kufuata haki miongoni mwa watu wa familia ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ndiye ambaye ana sifa za waumini, anastahiki kuombewa na kutakiwa radhi. Lakini hata hivyo hawavuki mipaka kwao. Wanazitambua fadhila zao, kwamba wao ndio waislamu bora kabisa na wana nafasi yenye kujulikana mbele ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah." (Sharh al-´Aqiydah al-Waasitwiyyah, uk. 72-73)

[8] Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah (Rahimahu Allaah) amesema:

"Hakuna aibu kwa yule mwenye kudhihirisha madhehebu ya Salaf, akajinasibisha nayo na akarejea kwayo. Bali ni wajibu kumkubalia hilo kwa makubaliano kwa sababu madhehebu ya Salaf si jengine isipokuwa ni haki" (Majmuu´-ul-Fataawaa (04/149))

Shaykh Bakr Abu Zayd (Rahimahu Allaah) amesema:

"Inaposemwa Salaf, Salafiyuun au mfumo wao ambao ni Salafiyyah, inahusiana na ujinasibishaji na Maswahabah (Radhiya Allaahu ´anhum) na wale wenye kuwafuata kwa wema pasina yule aliyepinda katika matamanio yake... Wale walioshikamana imara na mfumo wa kiutume ananasibishwa na watangu wake wema katika hilo. Ndio maana wanaitwa "Salaf" na "Salafiyyuun". Yule mwenye kujinasibisha na wao anaitwa "Salafiy". Kutokana na hilo neno Salaf ni wale wema waliotangulia. Msemo huu unajumuisha kila yule mwenye kuwaiga Maswahabah (Radhiya Allaahu ´anhum) ikiwa ni pamoja na watu wa leo, hivyo ndivyo wanavosema wanachuoni. Sio unasibishaji wa mielekeo inayoenda kinyume na Qur-aan na Sunnah. Sio unasibishaji ambao kwa wakati hata mmoja umeenda kinyume na karne za kwanza; bali umetoka kwao na pamoja nao. Pamoja na hivyo mtu hawezi kusema hivo kwa wale walioenda kinyume nao kwa jina au mwelekeo hata kama wataishi baina yao na wao." (Hukm-ul-Intimaa´, uk. 46)

9- Hatukubali vitabu vya Fiqh, vitabu vya Tafsiyr ya Qur-aan, visa vya zamani, historia ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) isipokuwa tu kile kilichothibiti kutoka kwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Haina maana kwamba tunavipinga au tunasema kuwa ni wenye kujitosheleza navyo, bali tunafaidika na zile hukumu walizofikia wanachuoni wetu, wasomi wa Fiqh na wengineo. Lakini hata hivyo hatuikubali hukumu yoyote isipokuwa kwa dalili sahihi.

10- Hatuandiki katika vitabu vyetu, hatutoi katika darsa zetu na wala hatukhutubu isipokuwa kwa Qur-aan na Hadiyth yenye kustahiki kutumiwa kama hoja. Kadhalika tunachukia vile vya batili na Hadiyth dhaifu na zilizotungwa, jambo ambalo linafanywa na waandishi na watoa mawaidha wengi.

11- Hatumkufurishi muislamu yeyote kwa dhambi isipokuwa pale atapomshirikisha Allaah, ataacha swalah[10] au ataritadi - Allaah atulinde sisi na nyinyi kutokamana na hayo.

12- Tunaamini kuwa Qur-aan ni maneno ya Allaah na hayakuumbwa[11].

---

[9] Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah (Rahimahu Allaah) amesema:

"Mimi daima hutambua kuwa mantiki ya kigiriki mwerevu haihitajii kama ambavyo vilevile haiwezi kumnufaisha mpumbavu." (Majmuu´-ul-Fataawaa (3/52))

[10] Imaam Muhammad bin Swaalih bin ´Uthaymiyn (Rahimahu Allaah) amesema:

"Asiyeswali ni mbaya zaidi kuliko mayahudi na manaswara. Mayahudi wakichinja mtu ameruhusiwa kula vichinjwa vyao. Manaswara wakichinja mtu ameruhusiwa vilevile kula vichinjwa vyao. Kuhusiana na mtu asiyeswali lau atachinja sio halali kula kichinjwa chake.

Mtu asiyeswali kwa mfano akiwa ni mwanamke sio halali kwa muislamu kumuoa. Upande mwingine akiwa ni mnaswara inajuzu kwa muislamu kumuoa. Vivyo hivyo akiwa ni myahudi inajuzu kwa muislamu kumuoa.

Mtu ambaye haswali hakubaliwi akaendelea kuacha swalah. Bali ataambiwa aswali la sivyo tunakuua. Upande mwingine myahudi na mnaswara anakubaliwa kubaki katika dini yake ima kwa kupeana ahadi, kumpa amani au mkataba." (Sharh Riyaadh-is-Swaalihiyn (05/99-100)

[11] ´Allaamah ´Abdul-´Aziyz bin ´Abdillaah ar-Raajhiy (Hafidhwahu Allaah) amesema:

"Qur-aan ni maneno ya Allaah (´Azza wa Jall) na sifa miongoni mwa sifa Zake. Allaah amezungumza kwa Qur-aan na akaiteremsha kwa Mtume wake Wahy.

13- Tunaona kuwa ni wajibu kusaidiana na muislamu yeyote katika haki. Tunajiweka mbali kwa Allaah kutokamana na wito wa kipindi cha ushirikiana kabla ya kuja Uislamu.

14- Hatuonelei kufaa kuwafanyia uasi watawala wa Kiislamu midhali bado ni waislamu. Kadhalika hatuoni kuwa kufanya mapinduzi ni njia ya kutengeneza. Uhakika wa mambo ni kwamba linaziharibu jamii. Kuhusiana na viongozi wa Aden tunaona kuwa inafaa kuwapiga vita ni jambo la wajibu mpaka watubu kutokamana na ukanajimungu, ujamaa, na kuwalingania kwao watu kuabudu [kaburi la] Lenin na Marx na vigogo wengine wa kikafiri.

15- Tunaona kuwa haya makundi mengi yaliyopo hii leo ndio sababu ya kuwafarikisha waislamu na kuwafanya wakawa madhaifu[12].

16- Tunaona kuwa ulinganizi wa al-Ikhwaan al-Muslimuun hauwezi na haustahiki kuinyoosha jamii. Kwa sababu imekuwa ni ulinganizi wa kisiasa na sio wa kiroho. Kunaingia vilevile Da´wah nyenginezo zilizozushwa. Ni Da´wah zinazoita kumpa kiapo cha usikivu na utiifu mtu asiyejulikana na ni za fitina. Da´wah hizi zimejengwa na zinaendeshwa kwa ujinga. Tunawanasihi baadhi ya ndugu wenye kuhusika nazo waachane nazo ili wakati wao usije kupotea bure katika mambo yasiyonufaisha Uislamu na

Qur-aan haikuumbwa kama wanavosema Ahl-ul-Bid´ah. Vilevile sio maana iliosimama katika nafsi yake. Bali ni maneno ya Allaah amezungumza kwayo, kwa Herufi na Sauti yenye kusikika. Aliisikia Jibriyl na Allaah akazungumza na Muhammad (Swala Allaahu ´alayhi wa sallam) usiku wa Mi´raaj na Muusa vilevile alisikia maneno ya Allaah. Hii ndio haki waliyomo wafuasi wa Mitume ambao ni Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah; Maswahabah, Taabi´uun na waliokuja baada yao." (al-Hidaayah ar-Rabbaaniyyah fiy Sharh al-´Aqiydah at-Twahaawiyyah (01/153-154)

[12] Aliulizwa Imaam Swaalih bin Fawzaan al-Fawzaan (Hafidhwahu Allaah) juu ya makundi ifuatavyo:

Swali 7: Unasemaje kuhusu makundi kwa hukumu ya jumla?

Jibu: Kila mwenye kwenda kinyume na Ahl-us-Sunnah ni mpotevu. Tuna kundi limoja tu nalo ni Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah. Mwenye kwenda kinyume na kundi hili anaenda kinyume na mfumo wa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

Vilevile kila mwenye kwenda kinyume na Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah ni katika Ahl-ul-Ahwaa´. Uhalifu huu unatofautiana inapokuja katika kusema kuwa mtu ni mpotevu au ni kafiri kwa kutegemea ukubwa wa uhalifu na umbali wa haki. (al-Ajwibah al-Mufiydah ´an As-ilat-il-Manaahij al-Jadiydah, uk. 28)

waislamu. Hamu kubwa ya muislamu iwe ya kwamba Allaah ataunusuru Uislamu na waislamu.

17- Kuhusiana na Jamaa´at-ut-Tabliygh[13], hebu pokea yale yaliypokelewa na ndugu muheshimiwa Muhammad bin ´Abdil-Wahhaab al-Wasswaabiy (Rahimahu Allaah) pale aliposema:

Mosi: Wanatendea kazi Hadiyth ambazo ni dhaifu. Sivyo tu, bali na zilizotungwa na zisizokuwa na msingi.

Pili: Wana Bid´ah chungunzima. Uhakika wa mambo ni kuwa ulinganizi wao umejengwa juu ya Bid´ah. Msingi na tawi la ulinganizi wao ni vikomo vya kutoka siku tatu kila mwezi, siku arubaini kila mwaka, miezi mine maishani, kufanya vikao viwili kila wiki; kikao kimoja kinafanywa kwenye msikiti ambao wanaswalia na kikao cha pili kwenye msikiti mwingine. Kila siku wanafanya halaka mbili; halaka moja inafanywa kwenye msikiti wanaoswalia

[13] Muftiy wa Saudi Arabia alotangulia na kichwa cha maqaadhiy na wa mambo ya Kiislamu Shaykh Muhammad bin Ibraahiym Aal ash-Shaykh (Rahimahu Allaah) amesema:

"Hakuna kheri yoyote kwenye jumuiya hii. Ni jumuiya ilio na Bid´ah na upotevu. Baada ya kusoma vijitabu vilivyoambatanishwa, tumekuta vina upotevu, Bid´ah na propaganda za kuabudu makaburi na shirki, jambo ambalo haliwezi kunyamaziwa.

Hivyo basi - Allaah Akitaka - tutalikemea na kufichua upotevu wake na kuraddi batili zake." (Majmuu´-ul-Fataawaa war-Rasaa-il (01/267))

Muftiy wa Saudi Arabia alotangulia Shaykh ´Abdul-´Aziyz bin Baaz (Rahimahu Allaah) amesema:

"Jamaa´at-ut-Tabliygh hawana umaizi katika ´Aqiydah. Haijuzu kutoka nao ikiwa mtu hana elimu na umaizi wa ´Aqiydah ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah ili mtu aweze kuwanasihi na kuwaelekeza na kushirikiana katika wema." (ad-Da´wah (1438) (1414-11-03)).

Amesema pindi alipoulizwa kama wanaingia katika mapote sabini na mbili [yatayoingia Motoni]:

"Ndio, wanaingia katika mapote sabini na mbili. Mwenye kwenda kinyume na ´Aqiydah ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah anaingia katika mapote sabini na mbili." (as-Salafiyyah (07/47) (1422)).

´Allaamah na Shams Muhaddith Shaykh Muhammad Naaswir-ud-Diyn al-Albaaniy (Rahimahu Allaah) amesema:

"Jamaa´at-ut-Tabliygh haikujengwa juu ya mfumo wa Qur-aan, Sunnah na Salaf. Hivyo haijuzu kutoka nao… " (al-Fataawaa al-Imaaraatiyyah).

na halaka nyingine inafanywa nyumbani. Hawako radhi na mtu isipokuwa mpaka ashikamane na mambo haya.

Hakuna shaka yoyote juu ya kwamba mambo haya ni Bid´ah katika dini. Ni mambo ambayo Allaah hakuteremsha dalili yoyote juu yake.

Tatu: Wanaona kuwa kuwalingania watu katika Tawhiyd kunawakimbiza watu.

Nne: Wanaona kuwa kuwalingania watu katika Tawhiyd pia kunawakimbiza watu.

Tano: Kiongozi wao Hudaydah anasema: "Bid´ah inayowakusanya watu ni bora kuliko Sunnah inayowafarikisha.""

Sita: Wana uadui kwa Ahl-us-Sunnah.

Saba: Wanawapuuzisha watu na elimu yenye manufaa. Wanafanya hivo kwa siri na kwa dhahiri.

Nane: Wanaona kuwa hakuna kufaulu kwa watu isipokuwa kupitia mfumo wao na wanalipigia hilo mfano kwa safina ya Nuuh. Mwenye kupanda katika safina hiyo, basi ameokoka, na asiyepanda, basi ameangamia. Nimejisikilia hilo mwenyewe Jordan na Yemen.

Tisa: Wanaipuuzia Tawhiyd-ul-Uluuhiyyah na Tawhiyd-ul-Asmaa´ was-Swifaat.

Kumi: Hawako tayari kujifunza elimu. Wanaona kuwa wakati unaotumiwa kujifunze elimu ni kupoteza muda.

Wana mengi mbali na yaliyotajwa.

18- Tumejifungamanisha katika uelewa wetu na Qur-aan na Sunnah kwa ufahamu wa Salaf wa Ummah huu katika Muhaddithuun. Hatumfuati kichwa mchunga mtu mmoja. Tunachukua haki kwa yeyote aliyekuja nayo. Vilevile tunajua kuwa kuna ambao wanadai Salafiyyah ilihali Salafiyyah haina lolote kabisa kuhusiana na wao. Kwa sababu watu kama hao wamekuwa ni wenye kuipaka jamii mafuta katika kuhalalisha yale aliyoharamisha Allaah. Kwa mfano ´Abdur-Rahmaan ´Abdul-Khaaliq na Muhammad Suruur.

19- Tunaamini kuwa siasa ni sehemu katika dini. Wale wanaojaribu kuitenganisha dini na siasa basi wanajaribu kuiharibu dini na kueneza vurugu. Kuhusu yaliyoenea katika baadhi ya miji ya Kiislamu ya kwamba:

"Dini ni ya Allaah na nchi ni ya wote."

ni wito wa kipindi cha kikafiri. Vyote viwili ni vya Allaah.

20- Tunaamini kuwa waislamu hawatotukuzwa na kunusuriwa mpaka warudi katika Kitabu cha Allaah na Sunnah za Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

21- Tunachukia mapote ya leo; pote la kikomunisti ni la kikafiri, pote la al-Ba´th ni la kikafiri, pote la Naaswir ni la kikafiri, pote la kijamaa ni la kikafiri na pote la Raafidhwah ni la kijambazi. Tunaona kuwa watu wamegawanyika mapote mawili:

Pote la Allaah: Ni wale ambao wanatendea kazi nguzo za Uislamu na nguzo za imani pasi na kurudisha kitu katika Shari´ah ya Allaah.

Pole la shaytwaan: Ni wale wenye kuipiga vita Shari´ah ya Allaah.

22- Tunawakemea wale ambao wanaigawanya dini kati ya mambo madogo na mambo ya msingi. Haya ni madai yenye kuangamiza.

23- Tunawakemea wale wenye kupuuza kujifuza Sunnah na wanasema kuwa sasa sio wakati wake. Kadhalika inahusiana na wale wenye kupuuzia na kutendea kazi Sunnah za Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa salla).

24- Tunaonelea kutanguliza mambo ambayo ni muhimu zaidi kuliko mengine. Ni wajibu kwa waislamu kutilia umuhimu mkubwa wa kuzitengeneza ´Aqiydah[14], kupambana na wakomunisti na kundi la al-Ba´th. Hayo hayapatikani isipokuwa kwa kuwa na umoja juu ya Qur-aan na Sunnah.

---

[14] ´Allaamah ´Abdul-´Aziyz bin ´Abdillaah ar-Raajhiy (Hafidhwahu Allaah) amesema:

Mja anaihitajia elimu hii - elimu ya somo la ´Aqiydah - juu ya haja zingine zote na dharurah yake iko juu ya dharurah zingine zote. Wanavyolihitajia ni zaidi ya wanavohitajia vyakula na kinywaji. Bali analitaji zaidi kuliko anavohitajia pumzi. Kwa sababu mtu akikosa chakula na kinywaji na pumzi mwili unakufa. Na mauti hakuna budi yatamfika tu. Haidhuru kitu mwili ukifa midhali moyo umenyooka. Upande mwingine mtu akikosa kumtambua Mola Wake, Majina na Sifa Zake na elimu kuhusu Shari´ah na Dini yake, basi moyo wake unakufa. Hapa ndipo kunabainika haja ya waja juu ya elimu ya msingi wa Dini. Hivyo ni kwa sababu hakuna uhai wa moyo, neema, utulivu wala furaha

isipokuwa kwa mja kumtambua Mola Wake, Mwumbaji Wake, Anayemwendesha na Anayemwabudu kwa Majina Yake na Sifa Zake. Kwa hayo atakuja kumpenda zaidi ya kila kitu na juhudi na matendo yake yatakuwa kwa yale yanayomkurubisha Kwake (Subhaanahu wa Ta´ala)." (al-Hidaayah ar-Rabbaaniyyah fiy Sharh al-´Aqiydah at-Twahaawiyyah (01/15)